# MKATABA WA UPANGAJI

**MKATABA HUU** umefanyika leo tarehe 1 mwezi Julai, 2024.

**Kati ya**

**TAUSI ALLY KITUNDU** simu namba **0754285845**, **ARUSHA** ambaye kwa maana ya mkataba huu ataitwa **'Mwenye Nyumba/ mpangishaji'** kwa upande mmoja,

**Na**

**NAHDY KENYA & TANZANIA SAFARIS LIMITED** kampuni iliyopo **ARUSHA** ambaye kwa maana ya mkataba huu ataitwa **'Mpangaji'** kwa upande mwingine.

**KWA KUWA**
Mwenye Nyumba ni mmiliki halali wa nyumba ambayo itatumika kama ofisi iliyopo Plot namba 40, Block namba 21, barabara ya Ngaramtoni, Mtaa wa Ngaramtoni ya Chini, Kata ya Olmoti, katika wilaya ya Arusha, mkoani Arusha.

**BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:-**

1. Kwamba Mwenye Nyumba anampangishia Mpangaji nyumba ambayo itatumika kama ofisi iliyopo Plot namba 40, Block namba 21, barabara ya Ngaramtoni, Mtaa wa Ngaramtoni ya Chini, Kata ya Olmoti, katika wilaya ya Arusha, mkoani Arusha ambayo kwa maana ya mkataba huu itaitwa 'Nyumba'.

2. Mwenye Nyumba ndiye, na ataendelea kuwa mmiliki halali wa nyumba ambayo itatumika kama ofisi iliyopo Plot namba 40, Block namba 21, barabara ya Ngaramtoni, Mtaa wa Ngaramtoni ya Chini, Kata ya Olmoti, katika wilaya ya Arusha, mkoani Arusha, nyumba ambayo ndani ya mkataba huu inatajwa kama ofisi.

3. Kwamba kipindi cha upangaji kitakuwa ni **Miaka Mitatu (3) (yaani kuanzia tarehe 1 mwezi Julai mwaka 2024 hadi tarehe tarehe 1 mwezi Julai mwaka 2027** na baada ya muda huu kuisha pande zote mbili zitaingia makubaliano mapya na masharti mapya ya upangaji kwa maandishi. Katika mkataba huu Mpangaji amelipa kodi ya miezi Sita (6) **ambayo ni kiasi cha Shilingi Milioni Nne na Laki Nane (Tshs. 4,800,000/=) ambapo kodi ya kila Mwezi ni kiasi cha Laki Nane (Tshs. 800,000/=) kwa Mwezi.**

4. Kwamba mara baada ya miezi sita kuisha pande zote mbili zitaingia makubaliano ya maandishi yaani kati ya Mwenye Nyumba na Mpangaji ambayo ni lazima yafanyike siku Thelathini kabla ya kuisha kwa kipindi cha Mkataba huu.

5. Mpangaji hataruhusiwa kupangisha kwa mtu awaye yoyote yule nyumba aliyokodisha bila idhini ya maandishi ya Mwenye Nyumba.

Said Amri
Box 16081 Arusha
Advocate, Notary Public

7. Kwamba Mpangaji haruhusiwi kufanya marekebisho yoyote au kuweka vitu vya kudumu kwenye nyumba bila idhini ya maandishi ya Mwenye Nyumba. Marekebisho au vitu vyovyote vya kudumu vitakavyowekwa kwenye nyumba vitakuwa ni mali ya Mwenye Nyumba baada ya mkataba kwisha bila Mwenye Nyumba kulipa fidia ya marekebisho hayo au vitu hivyo.

8. Kwamba Mpangaji atahakikisha kuwa wakati wote wa mkataba nyumba ikiwa ni pamoja na kuta na vitu vyote vilivyopo ndani kinakuwa katika hali nzuri.

9. Kwamba Mpangaji atawajibika kulipia bili za maji kadiri ya matumizi yake.

10. Kwamba Mpangaji haruhusiwi kufanya mambo/shughuli ambazo zitakuwa kero kwa majirani ndani ya nyumba. Vile vile ni marufuku kwa Mpangaji kuingiza madawa ya kulevya au (biashara yoyote haramu kwa mujibu wa sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania) kwenye nyumba.

11. Kwamba Mwenye Nyumba atakuwa na nafasi yakukagua nyumba baada ya kutoa taarifa ya mdomo ya siku mbili ilikuangalia hali ya nyumba.

12. Kwamba Mwenye Nyumba atakuwa na haki ya kumtoa Mpangaji na kufunga nyumba iwapo Mpangaji atakuwa amevunja sharti lolote katika mkataba huu au akikataa kuingia katika mkataba mwingine baada ya Mkataba huu kuisha.

13. Kwamba Mpangaji atamfidia Mwenye Nyumba kwa uharibifu atakaosababisha kwenye nyumba au kwa mtu mwingine yeyote kutokana na kitendo/uzembe wake au wa mfanyakazi au wakala wake.

14. Kwamba Mwenye Nyumba atahakikisha kuwa katika kipindi chote cha mkataba Mpangaji ataishi bila kubughudhiwa kama atatekeleza masharti yote ya mkataba na kutimiza masharti yote ya upangaji, mpangaji atakuwa huru kutumia nyumba cha biashara kwa ajili ya madhumuni yaliyoainishwa katika mkataba huu bila vikwazo vyovyote ambavyo niki nyume na mkataba.

15. Kwamba endapo Mpangaji atashindwa kutekeleza masharti ya mkataba huu baada ya kupewa notisi ya maandishi ya siku 30 Mwenye Nyumba atakuwa na haki ya kuingia kwenye nyumba na kumuondoa Mpangaji.

16. Kwamba Mwenye Nyumba hatawajibika kumlipa Mpangaji kutokana na hasara atakayopata kutokana na wizi wakati akiwa Mpangaji. Mpangaji atawajibika kuweka ulinzi kwenye nyumba kwa gharama zake mwenyewe.

17. Mpangaji atawajibika kufanya usafi ndani ya nyumba, mtaro wa nje, baraza, choo na usafi wote unaotakiwa kufanywa kwa mujibu wa taratibu za Serikali au Jiji la Arusha na endapo hatafanya hivyo atawajibika kulipa faini za serikali.

18. **TAARIFA** yeyote inayotakiwa katika mkataba huu ni lazima iwe kwa maandishi na itatolewa kwa Mpangaji kwa njia ya mdomo au kutumwa kwa njia ya simu iliyoandikwa kwenye mkataba huu.

Said Amri
Box 16091 Arusha
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

19. Kwamba pande zote zimeingia kwenye mkataba huu kwa hiari na zikiwa na akili timamu.

20. Kwamba mkataba huu unahusu pande mbili tu yaani Mwenye Nyumba na Mpangaji, hakuna upande unaoruhusiwa kuvujisha taarifa au masharti ya mkataba huu bila ridhaa ya upande wa pili wa mkataba huu.

**KWA USHUHUDA** na **UTHIBITISHO**, mkataba huu umewekwa sahihi na Mwenye Nyumba/mpangishaji na Mpangishaji mbele ya Wakili na mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini.

**MKATABA HUU** umesainiwa na **TAUSI ALLY KITUNDU** ambae ametabulishwa kwangu na Giftiel Mshana na kunamfahamu binafsi leo tarehe 1 mwezi Julai, 2024

---------------------------------
**MPANGISHAJI**

Wakili/Kamishna wa Viapo:
Jina Kamili: SAID AMRI

Sahihi: ____________________
Anuani: S.L.P 16081, ARUSHA
Cheo : WAKILI

Said Amri
Box 16081 Arusha
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Jina: **NUUMAN ABDALAH KASSIM** Sahihi.......................................
Wadhifa **MKURUGENZI** Simu: **0739085511**

**MKATABA HUU** umewekwa Muhuri/lakiri ya kampuni ya **NAHDY KENYA & TANZANIA SAFARIS LIMITED** ambae ninamfahamu binafsi leo tarehe 1 mwezi Julai, 2024

---------------------------------
MPANGAJI

NAHDY KENYA & TANZANIA SAFARIS LIMITED
P.O.BOX 15
01 JUL 2024
ARUSHA
TANZANIA

Wakili/Kamishna wa Viapo:
Jina Kamili: SAID AMRI

Sahihi: ____________________
Anuani: S.L.P 16081, ARUSHA
Cheo : WAKILI

Said Amri
Box 16081 Arusha
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths